



Benki Ya Dunia

Makhtar Diop **Makamu wa Rais, Kanda ya Afrika**



Makhtar Diop ni Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia wa Kanda ya Afrika tangu Mei 6, 2012.

Kabla ya kuchukua wadhifa huu, alikuwa Mkurugenzi wa Benki ya Dunia wa nchi ya Brazili kati ya Januari 2009 na Aprili 2012, na hapo awali alishikilia wadhifa wa Mkurugenzi wa Mkakati na Shughuli za Amerika ya Kusini na Kanda ya Caribbean, na Mkurugenzi wa Sekta ya Kifedha, Sekta ya kibinafsi na Miundombinu kwenye kanda hilo.

Kati ya 2002 na 2005 Bwana Diop alikuwa Mkurugenzi wa Benki ya Dunia wa nchi ya Kenya, Eritrea, na Somalia.

Kabla ya kujiunga na Benki ya Dunia, Bwana Diop alifanya kazi katika Shirika la Fedha Duniani, na alihudumu kama Waziri wa Uchumi na Fedha huko Senegal.